

## **MAELEKEZO YA MATUMIZI YA KIFAA CHA KUKUSANYA SAMPULI YA CHOO**

MUHIMU: Tafadhali soma na ufuate maelekezo yote.

**TAHADHARI: MAJIMAJI YALIYO KWENYE TYUBU YANA SUMU, USINYWE**

Umepewa kifaa cha kukusanya ambacho kitakusaidia kukusanya sampuli ya choo kwa urahisi. Maelekezo haya yatakusaidia kutumia kifaa. Hii itasaidia maabara kufanya kazi njema na kuepuka upimaji wa kurudia wenyewe gharama kubwa.

Kifaa hiki kina tyubu 1, 2 au 3. Tyubu hizo zinaweza kuwa au kutokuwa na majimaji ndani yake. Tafadhali kumbuka kwamba kuna maelekezo tofauti ya ukusanyaji kwa tyubu zilizo na majimaji na zile ambazo hazina majimaji. Majimaji hayo yana sumu. Usiyanywe. Ziweke mbali na mahali ambapo watoto wanawenza kufikia.

Unapaswa kuweka kila mkusanyiko wa sampuli katika tyubu tofauti. Tafadhali ruhusu saa 12-24 kati ya kila mkusanyiko wa choo.

Kabla ya kuanza, tafadhali kumbuka yafuatayo:

USIKOJOE kwenye sampuli au katika kontena ya kuhifadhi sampuli.

USIKOJOE kwenye tyubu.

USIWEKE sampuli kwenye tyubu moja kwa moja.

USIWEKE sampuli kwenye msala.

Kusanya sampuli kama ulivyoelekezwa hapa chini.

Ruhusu saa 12-24 kati ya kila mkusanyiko wa sampuli.

1. Ukianza kukusanya sampuli, tafadhali kumbuka kwamba CHOO hakiwezi kuweka kwenye kichupa kilichotolewa moja kwa moja. Choo hicho kinapaswa kuweka kwenye kontena safi ILIYOKAUZA badala yake. Kwa mfano, unaweza kuweka mfuko mkubwa wa plastiki kwenye kikapu cha takataka ili kunasa sampuliu utumie kontena au chupa kubwa ambayo ni safi. Tafadhali kumbuka: mkojo HAUWEZI kuchanganywa na sampuli hii.
2. Pindi baada ya choo kuweka kwenye kontena safi iliyokauka, fungua tyubu iliyo na majimaji. Ukitumia kijiko cha kukusanya kilicho kwenye kifuniko cha tyubu (au vijiti vyta mbao, iwapo vimetolewa), weka vijiko vidogo vyta choo kutoka kwa maeneo yanayoonekana kuwa na damu, utelezi au maji ndani ya tyubu hadi kifike katika mstari mwekundu. Ikiwa choo ni kigumu, tafadhali jaribu kuteua kiasi kidogo kidogo kutoka kila eneo la mwisho na katikati.
3. Changanya mkusanyiko ulio kwenye tyubu kwa kijiko au kijiti cha mbao, kisha ufunge kifuniko kabisa na kutikisa tyubu kwa nguvu hadi mkusanyiko uliomo uchanganyike vyema.
4. Rudia maelekezo ya 1, 2 na 3 kwa kila tyubu iliyo na majimaji tu. Kabla ya kurudia, tafadhali hakikisha kwamba unaruhusu saa 12-24 kati ya kila mkusanyiko wa sampuli. Hifadhi vichupa hivi katika halijoto ya kawaida.
5. Ikiwa mojawapo ya tyubu zilizotolewa haina majimaji ndani yake, ijaze kwa choo hadi kwa mstari mwekundu, lakini USICHANGANYE au kutikisa tyubu hii. WEKA KICHUPA HIKI CHENYE KIFUNIKO CHEUPE PEKEE KWENYE FRIJI. Kama ilivyoelezwa hapa juu, hifadhi vichupa vingine vyote kwenye halijoto ya kawaida.

6. Weka lebo kwenye tyubu kwa maelezo tambulishi yaliyoombwa. Pia tia alama kwenye kisanduku kilicho kwenye lebo kinachoonekana kama sampuli zaidi inapokusanya (tazama kielelezo).
7. ANGALIA VIFUNIKO VYOTE VYA VICHUPA ILI KUHAKIKISHA KWAMBA VIMEFUNKWA KABISA.
8. Osha mikono yako vyema. Ikiwa majimaji yoyote kutoka kwa tyubu yatagusa ngozi yako au kuingia machoni, osha kwa maji mengi yanayotiririka. Ikiwa utaanza kuwashwa, tafuta ushauri wa daktari.
9. Baada ya sampuli zote kukusanya, ziweke kwenye begi au katoni ili kuwasilishwa kwa daktari au maabara. Tia alama kwenye lebo iliyo kwenye katoni au begi kwa maelezo yanayohitajika kama vile jina lako, tarehe ya kuzaliwa, jinsia na anwani ya nyumbani.
10. Rejesha kifaa cha kukusanya kwa daktari wako au maabara.

**IKIWA YATAMEZWA:** Zimua kwa kunywa glasi 2-4 za maji na uwasiliane nakituo cha dharura, kituo cha maelezo kuhusu sumu au utembelee daktari ili kupokea matibabu mara moja. Hifadhi tyubu ambayo ulikunyuwa majimaji yake: weka lebo kwa maelezo ambayo yatakuwa muhimu katika kubainisha matibabu yanayofaa.